PAN AFRICAN PARLIAMENT

PARLEMENT PANAFRICAIN

البرلمان الأفريقي

PARLAMENTO PAN-AFRICANO

# Kufanya Uwekezaji kuwa wa Manufaa kwa Afrika: Jibu la Mbunge kuhusu "Unyakuzi wa Ardhi"

Julai 21–22, 2011

Bunge la Afrika, Midrand, Afrika Kusini

---

Ripoti kutoka kwa semina juu ya uwekezaji wa kigeni katika ardhi ya kilimo na maji, iliyoandaliwa na Bunge la Afrika kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (IISD) na Taasisi ya Taaluma ya Umaskini, Ardhi na Kilimo (PLAAS).

Semina iliweza kuendeshwa kwa msaada kutoka kwa Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ).

oktoba 2011

Kufanya Uwekezaji kuwa wa Manufaa kwa Afrika: Jibu la Mbunge kuhusu "Unyakuzi wa Ardhi"

# *DIBAJI NA JOAQUIM ALBERTO CHISSANO, ALIYEKUWA RAIS WA MSUMBIJI NA MWENYEKITI WA JUKWAA LA AFRIKA*

*"Niliubana mkono wa babangu na kumwambia nitalilinda kaburi lake kwa maisha yangu.*
*Baba akatabasamu na kuaga dunia akajiendea ulimwengu wa miungu."*

*Chifu Joseph wa Wal-lam-wat-kain (Wallowa) Mhindi mwanaharakati wa Kibinadamu na mweka amani Machi 3, 1840 – Septemba 21, 1904*

Ripoti kutoka kwa semina iliyoitwa, Kufanya Uwekezaji kuwa wa Manufaa kwa Afrika, iliyoandaliwa na Bunge la Afrika katika Midrand, Afrika Kusini kuanzia Julai 21-22, 2011, ina mapendekezo muhimu juu ya njia nzuri ya kutekeleza madhumuni makuu ya Azimio la Maputo kuhusu kujifungia kwa Mpango Mpana wa Maendeleo ya Kilimo katika Afrika (CAADP), ambalo lilipitishwa jijini Maputo, Jamhuri ya Msumbiji, mnamo 2003. Semina, ya kwanza ya aina yake, iliandaliwa kwa ushirikiano na Taaisi ya Kimataifa kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (IISD) na Taasisi ya Taaluma ya Umaskini, Ardhi na Kilimo (PLAAS), ilihudhuriwa na wabunge 40, wawakilishi kutoka wakala wa wanaohudumu katika zaidi ya nchi moja kama vile Umoja wa Afrika (UA) na Wakala wa Mipango na Uratibu wa NEPAD, Tume ya Kiuchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika (UNECA), Benki ya Maendeleo ya Afrika, jumuia ya wafadhili, wasomi na jumuia ya kiraia. Mchango mzuri pia ulitolewa na Sekretariati ya Hatua ya Sera ya Ardhi (LPI) ya UA-ECA-AfDB.

Jukwaa la Waafrika Waliokuwa Wakuu wa Nchi na Serikali, lilifurahia kualikwa kwa semina hiyo. Jukwaa la Afrika lingependa kusisitiza tena kujitolea kwa wanachama wake kutumia uzoefu wao, maarifa, utaalamu, ofisi na mamlaka kimadili ili kukuza na kukinga uongozi kidemokrasia, kanuni na maadili, pamoja na kuchangia ujenzi wa nchi endelevu za Kiafrika. Kwa hivyo, Jukwaa la Afrika linashukuru sana kwa fursa lililopata ya kushiriki katika semina. Waama, semina ilitaarifu na kufaidi, hasa kuhusiana na dhima inayotekelezwa na Bunge la Afrika katika kutoa jukwaa la kutafakari juu ya ajenda ya Afrika juu ya maendeleo na ustawi endelevu.

Ripoti hii inatoa maelezo ya jumla juu ya uwekezaji wa kigeni katika ardhi ya kilimo na maji. Dhana ya kuliamsha jitu la Afrika lililolala, kama ilivyodaiwa na Benki ya Dunia, inaendelea kuwa ya kweli. Kwa hakika, takwimu zilizopo zinaonyesha dhahiri shahiri kwamba washirika wa kimataifa kutoka kwa sekta za umma na binafsi wanalenga macho kwa Afrika ili kusuluhisha mahitaji yao ya chakula na nishati. Kwa kweli, kuhusiana na suala la ardhi na kilimo, Afrika inaendelea kiutaratibu kuwa "bara la siku zinazokuja". Mapatano ya Kimataifa kuhusu Ardhi yanakadiria kwamba hekta milioni 80 za ardhi zimetolewa kwa wawekezaji katika miaka iliyopita, ambapo hekta milioni 50 kati ya hizo ziko katika Afrika pekee. Suala la unyakuzi wa ardhi katika Afrika si uwongo. Ni ukweli. Sasa ni wakati kwa Afrika kuanza mjadala na mashauriano mapana juu ya sera mwafaka za ardhi na miundo kisheria, ambapo mabunge yana nafasi muhimu katika usanifu na utelekelezaji wao.

Kwa hivyo, ni muhimu kuchukulia kwa makini mapendekezo ya semina, hasa katika muktadha wa utekelezaji kwa ujumla wa CAADP. Ni matumaini na matarajio yetu kwamba semina haikuwa shughuli ya kufanywa mara moja tu, bali ni mwanzo wa msululu wa warsha za sera ili kukuza ufahamu wa umma juu ya umuhimu wa ardhi ya kilimo na maji katika juhudi za maendeleo ya Afrika. Jukwaa la Afrika lingependa kulihimiza Bunge la Afrika kuendelea kushauriana na washirika wake, hasa, UA, UNECA na AfDB kupitia kwa Sekretariati ya Hatua ya Sera ya Ardhi pamoja na msaada kimafunzo kutoka kwa IISD na PLAAS kwa nchi za Kiafrika, kwa kusudi la kufanya uwekezaji kuwa wa manufaa kwa Afrika.

Joaquim Alberto Chissano
Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Msumbiji
Mwenyekiti wa Jukwaa la Afrika

AFRICA FORUM

JUKWAA LA WALIOKUWA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI ZA AFRIKA

## *Yaliyomo*

Utangulizi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Moussa Idriss Ndélé, Rais wa Bunge la Afrika ..................... 1

Maelezo ya Jumla kuhusu uwekezaji wa Kigeni katika Ardhi ya Kilimo na Maji .................................. 2

Ni nani wawekezaji? ..................................................................................................... 3

Kutathmini Athari katika Afrika ..................................................................................... 4

Athari Kisheria kwa Uwekezaji wa Kigeni ....................................................................... 6

Hatua za Umoja wa Afrika na za kiulimwengu kuhusu kilimo, maendeleo ya mashambani, ardhi na maji ........................................................................................................... 8

Uwekezaji wa Kilimo Kiumma na Kibinafsi: kutekelea Azimio la Maputo ............................................ 9

Nafasi ya Wabunge ..................................................................................................... 11

Mapendekezo na hatua fuatilizi ..................................................................................... 12

Rasimu ya Azimio ....................................................................................................... 13

## *Utangulizi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Moussa Idriss Ndélé, Rais wa Bunge la Afrika*

Wimbi jipya la uwekezaji wa kigeni katika ardhi ya kilimo na maji ya Afrika lilianza mnamo 2008 kufuatia ongezeko la mahitaji ya fueli za bio, ongezeko la bei za mafuta, janga kuu la chakula na kudororoa kwa uchumi duniani katika Ulaya na Amerika Kaskazini. Habari zilizosambaa katika vyombo vya habari na msululu wa tafiti zilizoendeshwa na Umoja wa Mataifa, Benki ya Dunia, vyuo vikuu na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, imethibitisha kiwango na athari za uwekezaji huo wa kigeni. Katika ripoti yake *Ongezeko la Upendeleo katika Ardhi ya Kilimo (Rising Global Interest in Farmland)*, Benki ya Dunia iliripoti kwamba biashara za ardhi katika Afrika zilihusu hekta milioni 32 katika mwaka 2009 pekee, na ukubwa huu unazidi jumla ya eneo la ardhi la Ghana au Uingereza. Nchi zilizokodisha ardhi kubwa zaidi kwa wawekezaji ni Sudan (hekta milioni 4), Msumbiji (hekta milioni 2.7), Liberia (hekta milioni 1.6) na Ethiopia (kati ya hekta milioni 1.3 na 3.6).

Raia wa Afrika milioni 832 wanawakilisha 13% ya watu wote duniani lakini wanachangia 1% ya pato ghafi la ndani duniani na 2% ya biashara ya dunia. Kwamba watu wengi wanaishi kwa chini ya dola moja kwa siku hadi sasa ni kizuizi kikubwa kwa maendeleo. Zaidi ya 70% ya watu maskini wanaishi katika maeneo ya mashambani na wanategemea kilimo ili kujikimu kimaisha.


Uwekezaji katika kilimo ni muhimu ili kuboresha njia ya kujipatia riziki mashinani. Vyanzo vipya vya uwekezaji vinaweza kuunga mkono dai la Wakuu wa Nchi na Serikali la 2003 katika Azimio la Umoja wa Afrika la Maputo ambapo walijitolea "kutoa mgao wa 10% wa raslimali za bajeti ya taifa kwa kilimo na utekelezaji wa sera ya maendeleo ya mashinani katika kipindi cha miaka mitano"

Kama jibu lake kwa ustawi wa uwekezaji wa kigeni moja kwa moja kwa kilimo na athari zake kwa watu wenye hatari ya kuathiriwa zaidi, Bunge la Afrika katika Mkutano wake wa Kawaida wa Tatu mnamo Oktoba 2010 lilipitisha mapendekezo ya Kamati ya Kudumu kuhusu Kilimo, Uchumi Mashinani, Raslimali Asili na Mazingira (CRENRE), kutoa kipaumbele kwa masuala ya uwekezaji katika ardhi ya kilimo na athari yake kwa usalama wa chakula na amani, ikiwa ni pamoja na:

- Kwamba uendeshwe uhisishaji juu ya unyakuzi wa ardhi kupitia warsha na mikutano ya kikanda na kibara ili kuwafahamisha wabunge na raia kuhusu suala hili;
- Kwamba kibuniwe chombo kinachowajumuisha Mawaziri wa Afrika kuhusu Ardhi ambacho ni cha kiwango kama kile kinachojumuisha Mawaziri wa Afrika wanaohusika na Mazingira (AMCE) na Baraza la Mawaziri wa Maji;
- Kwamba maagizo kuhusu usimamiaji bora wa ardhi yastawishwe ili kusaidia utekelezaji wa Muundo wa Umoja wa Afrika na Miongozo ya Sera ya Ardhi, kama ilivyopitishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali jijini Tripoli mnamo Juni 2009;
- Kwamba kanuni kuhusu uwekezaji huu maalum ziundwe ili kulinda faida za uwekezaji huu kwa nchi za Afrika na raia wake.

Ni furaha yangu kutangaza kwamba juhudi hizi sasa zimeanza. Semina ya kwanza iliandaliwa katika Bunge la Afrika mnamo Julai 21–22, 2011. Wabunge arubaini, wawakilishi wa wakala wa serikali mbalimbali wakiwemo Umoja wa Afrika na NEPAD, UNECA, jumuia ya wafadhili, wasomi na jumuia za kiraia walihudhuria semina hiyo. Hatua ya kwanza ililenga dhima ya Bunge la Afrika kutoa jukwaa la pamoja kwa watu wa Afrika na miungano yao ya mashinani, kuhusika zaidi katika mijadala na kufanya maamuzi juu ya matatizo na changamoto kwa bara. Ninafurahi kwamba ni Bunge la Afrika lililoanzisha mjadala huu. Matokeo ya mjadala huu ambayo yanafuata hapo chini yataunda njia ya kufuatwa na vitendo zaidi kote barani. Tuna matumaini ya kuipanua hatua hii kwa ushirikiano nanyi na michango yenu. Ninawatakia waandalizi ufanisi.

Afrika Moja, Sauti Moja.



Mheshimiwa Dkt. Moussa Idriss Ndélé
Rais wa Bunge la Afrika

## *Maelezo ya Jumla kuhusu uwekezaji wa Kigeni katika Ardhi ya Kilimo na Maji*

Mnamo 2009, Benki ya Dunia ilichapisha ripoti, *Kuamsha Jitu Lililolala la Afrika (Awakening African's Sleeping Giant)*, ambayo ilidai kwamba uzalishaji wa chakula duniani itabidi uongezeke mara dufu kufikia mwaka 2050 ili kukidhi mahitaji, na kwamba wadau wa kimataifa kutoka kwa sekta za umma na kibinafsi, wanastahili kutazama Afrika ili wasuluhishe matatizo yake ya chakula na nishati. Kwa hakika, wimbi jipya la uwekezaji katika kilimo lilivuma. Lengo kuu lilikuwa ni kujipatia hati za kumiliki ardhi, maji na raslimali asili nyingine, zilizohitajika ili kukuza mazao ya chakula, nishati na vyakula vya wanyama. Hali hii inabadilisha kwa kasi taswira ya jamii za mashinani na aghalabu hii huwa inaitwa "unyakuzi wa ardhi."

Mnamo 2010, Benki ya Dunia ilichapisha, *Ongezeko la Raghba ya Kidunia katika Ardhi ya Kilimo (Rising Global Interest in Farmland)*, chapisho ambalo lilitoa tathmini kitakwimu na kiustahilifu juu ya unyakuzi wa ardhi duniani. Walipata kuwa ripoti za mapatano mnamo 2009 zilikuwa hekta milioni 45 za ardhi, huku milioni 32 zikiwa ni katika Afrika pekee. Muungano wa Kimataifa juu ya Ardhi unakisia kwamba hekta milioni 80 za ardhi zimetolewa kwa wawekezaji katika miaka michache iliyopita, hekta milioni 50 zikiwa ni katika Afrika pekee. Unyakuzi wa hivi majuzi wa ardhi ya kilimo katika Afrika ulifanywa na wawekezaji wageni na wa hapa nyumbani haufanyiki kwa kuzingatia muktadha wa manufaa kimazingira na kijamii kwa Waafrika. Mikataba ya ardhi kimsingi huwa ni kwa miaka 55 hadi 99 na kwa jumla, miradi hii haileti faida kwa jamii au nchi, kupitia kwa nyongeza ya nafasi za ajira, uhawilishaji wa teknolojia, uboreshaji wa stadi au kujenga uwezo.

Afrika ndio inalengwa kwa sababu ya fikra kuwa: ina ardhi kubwa na maji, kutokuwepo au kuwepo kwa mifumo dhaifu ya umiliki wa ardhi na kufeli kwa serikali kulinda vilivyo watumiaji wa ardhi. Inakisiwa kwamba 80% ya ardhi katika Afrika ni ya dola na mojawapo ya migogoro kuhusiana na "unyakuzi wa ardhi" ni kwamba mamlaka ambazo hufanya mikataba ya kukodi ardhi si wenye ardhi au watumiaji wa ardhi, bali ni serkali za kitaifa. Iwapo pana fidia inayolipwa kwa wenye ardhi, aghalabu wao huwa hawauhusiani na thamani ya ardhi, kwa sababu wale wanaofanya ukadiriaji wa thamani ya ardhi ni mamlaka za serikali.

Motisha ya wimbi hili jipya la uwekezaji inaendeshwa kwa nguvu na haja ya maji. Uwekezaji umezunguka mabonde makuu ya mito, yakiwemo mabonde yafuatayo: Bonde la Mto Senegal, Bonde la Mto Nijaa na Bonde Kongo. Nchi zenye uhaba au raslimali maji zilizofyonzwa na kuachwa tupu zinatafuta njia ya kupata maji kutoka nje kwa kupanda mazao yao katika nchi za kigeni. Katika kongamano la uwekezaji jijini Geneva mnamo 2010, Judson Hill kutoka Kampuni ya NGP Global Adaptation, mfuko wa kibinafsi unaowekeza katika hisa alisema, "nchi inapoagizia tani moja ya ngano inaokoa karibu mita 1300 mchemraba za maji ya nyumbani." Kwa sababu hiyo, Afrika inasaidia, aghalabu bila malipo, kutimiza mahitaji ya maji ya nchi nyingine. Isitoshe, mkimbio huu mpya wa wawekezaji unatokea katika muktadha wa ongezeko la haraka la idadi ya watu katika bara la Afrika, ambalo juu yake pia lina ongezeko la kupungua kwa raslimali, jambo linalofanya kuwa vigumu kwa Afrika kukidhi mahitaji yake.

Bila shaka, ongezeko la uwekezaji ni nafasi kwa maendeleo ya kilimo na upungazji wa umaskini. Lakini ni muhimu pia kufikiri juu ya aina ya uwekezaji unaohitajika. Ni nani anastahili kuwekeza na ni wapi pesa zitatoka? Kwa mujibu wa Programu ya Dhati ya Uwekezaji katika Kilimo barani Afrika (CAADP), Afrika inahitaji uwekezaji wa dola 250 bilioni ili kustawisha miundo mbinu katika maeneo ya mashinani kati ya 2002 na 2015. Licha ya hayo, ni nchi chache sana zimeitikia Azimio la Maputo, na Usaidizi wa Maendeleo kutoka Nchi za Kigeni (ODA) na uhisani ungali finyu, hali ambayo imekuza utegemezi. Wawekezaji wakuu katika kilimo bado ni wakulima wadogo wadogo. Swali kuu ni: ni vipi tunaweza kuwaimarisha na ni vipi tunaweza kuwekeza ndani yao ili kuboresha uzalishaji na kiwango chao cha maisha? Je, mtindo wa sasa wa uwekezaji wa kigeni ndio jibu?



From left to right, Gaynor Paradza from the Institute for Poverty, Land and Agrarian Studies (PLAAS), Hon. Sisa James Njikelana from South Africa, Hon. Dr. Augustin Iyamuremye from Rwanda and Isilda Nhantumbo from the International Institute for Environment and Development. *Photo courtesy of Ruth Hall, PLAAS.*

## *Ni nani wawekezaji?*

Kuna aina tatu za wawekezaji ambao wanalenga ardhi ya kilimo na maji katika Afrika. Kwanza, nchi zenye utajiri wa pesa lakini zenye ukosefu wa usalama wa chakula, hasa nchi za Ghuba lakini pia nchi kutoka Ashia, ambazo kwa kiwango kikubwa zinategemea mifuko ya utajiri wa nchi na mashirika ya kibiashara yaliyomilikiwa na serikali. Pili, biashara za kilimo cha kijadi za nchi za magharibi zinazojihusisha na uzalishaji wa chakula, viwanda vya utengenezaji na uuzaji ng'ambo ambavyo vinatafuta jinsi ya kupanua nafasi zao za masoko. Na tatu, kundi jipya kutoka kwa sekta ya kifedha, zikiwemo benki, mifuko ya kibinafsi inayowekeza katika hisa na mifuko ya kinga na pensheni. Mifuko hii inaweza kuwa ya kibinafsi au ya umma. Mfuko wa Kilimo cha Afrika, kwa mfano, ni mali ya Wakala wa Maendeleo wa Ufaransa. Usimamiaji Ibuka wa mali ni mfuko wa kibinafsi ambao unafanya kazi katika zaidi ya nchi 18 zikiwemo Afrika Kusini, Msumbiji na Zambia.Kundi hili linaendeshwa hasa na nafasi za kufikirika za soko hili jipya linaloelekea kuwa na faida kubwa. Makampuni ya kusimamia mali hutunza mifuko hii, hununua ardhi kwa matumaini ya kupanda na kushuka kwa bei za ardhi na chakula.

Kundi la tatu la wawekezaji linabadilisha kimsingi muundo wa ardhi ya kilimo. Tunashuhudia mfumo wa kutoa fedha na kuleta ushirika katika sekta za kilimo kwa kutegemea mifumo ya biashara za ulanguzi. Kwa hakika, Oxfam imefanya utafiti katika Ethiopia, Ghana, Mali na Tanzania, na matokeo ya awali yanaonyesha kwamba chini ya 12% ya ardhi iliyonyakuliwa na wawekezaji imeanza kutumika, jambo linaonyesha ulanguzi wa hali ya juu.

## *Kutathmini Athari katika Afrika*

Tafiti za kina zimethibitisha kima na athari za uwekezaji wa hivi majuzi[1] katika kilimo. Matokeo yalijadiliwa kwa upana wakati wa semina na mahitimisho yaliyotolewa na wabunge pamoja na washiriki wengine, yanajumuisha:

1. *Haki za Ardhi zinadhoofishwa.* Barani Afrika, sehemu kubwa ya ardhi ni mali ya serikali, jambo ambalo ni urithi wa kikoloni; hii ina maana kwamba serikali inaamua jinsi ardhi hiyo inatumika. Haki za watu kwa ardhi zina utata, kwani zimejikita katika tamaduni au hazipo kabisa. Lakini, hakuna ardhi ya kilimo ambayo ni "wazi", "inayolala tu" au "isiyotumika" katika Afrika. Mapatano ya uwekezaji yaliyotiwa saini kati ya serikali na wawekezaji wa kigeni yanafanywa katika ardhi ambayo inatumiwa na watu, na hivyo kuathiri kihasi haki zao kwa ardhi, maji na raslimali nyingine. Hata katika nchi kama vile Msumbiji, ambayo inadhaniwa kuwa na mageuzi bora kabisa ya ardhi katika Afrika kwa sababu inatoa hati miliki kisheria kwa jamii, serikali ilitoa ardhi kwa wawekezaji wa kigeni katika maeneo ambapo jamii zilikuwa na hati miliki za kisheria. Nchini Ethiopia, ardhi yote iliyotolewa kwa wawekezaji wa kigeni, inadaiwa kwamba ilikuwa katika maeneo ya "ardhi taka", lakini kunao ushahidi sasa kwamba wakulima walihamishwa, hasa wakulima wa kuhama hama na wanaokuwa wafugaji nyakati za kuhama.
2. *Ukosefu Mkubwa wa uangavu.* Mapatano yanafanywa kisirsiri na yaliyomo katika mapatano hayo hayafichuliwi kwa umma. Kuna suala la undumakuwili kwa upande wa wawekezaji wa kimagharibi. Kwa upande mmoja, wanazungumzia uongozi bora katika Afrika kupitia mbinu kama vile uangavu na uwajibikaji, lakini wanaziruhusu kampuni zao kufikia mapatano na tena kisirisiri, jambo ambalo ni hatari kwa maslahi ya Afrika. Katika baadhi ya nchi wabunge wana sauti kwani ni lazima waidhinishe mapatano hayo. Lakini katika nchi nyingine nyingi hali sivyo hivi ilivyo. Wabunge wengi walilalamikia jinsi ilivyokuwa vigumu kwao kuona mapatano hayo. Nchini Tanzania, kwa mfano, wabunge wameiuliza serikali ifichue wazi mapatano hayo lakini kufikia sasa serikali haijaridhia.
3. *Wawekezaji wanazilenga nchi zenye sheria dhaifu.* Utafiti wa Benki ya Dunia uligundua kwamba wawekezaji walikuwa wanalenga nchi zenye sheria za ardhi dhaifu. Hali hii ni mbaya sana pale ambapo hakuna usawa katika uwezo wa kujadili juu ya mapatano kwani wawekezaji huwa na mawakili, wataalamu wa hali ya juu na uwezo mkubwa wa kujadili, kinyume na nchi za Afrika ambazo huwa katika hali dhaifu kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu. Vibaya zaidi ni pale ambapo wanaojadili huzungumza moja kwa moja na wamiliki wa ardhi ambao ni wakulima wenye elimu ya chini, wasiokuwa na uwezo wa kutetea maslahi yao. Hili lilikuwa suala la kusikitisha kwa wabunge wengi.
4. *Kuyafikia maji kunaingiliwa.* Wawekezaji hawatafuti tu ardhi bali muhimu zaidi ni kwamba wanatafuta raslimali maji zilizopo. Hali hii inaleta ushindani na watumiaji wa maji wa kiasili, hasa kutokana na wamiliki wa mashamba makubwa wanaotumia maji mengi na hivyo kupunguza kiwango cha upatikanji wa maji kwa ajili ya matumizi ya kinyumbani na kilimo.

[1] Tafiti ziliendeshwa na Muungano wa Chakula na Kilimo (FAO), Habari ya Chakulakwanza na Mtandao wa Vitendo (FIAN),Wakala wa Ujerumani kwa Ajili ya Ushirikiano Kimataifa (GIZ), Nafaka, Taasisi ya Kimataifa juu ya Utafiti wa Sera ya Chakula (IFPRI), Mfuko wa Kimataifa kwa ajili ya Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Taasisi ya Kimataifa kwa Mazingira na Maendeleo (IIED), Taasisi ya Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu (IISD), Muungano wa Kimataifa kuhusu Ardhi, Hatua ya Siasa za Mikataba ya Ardhi, Taasisi ya Oakland, Oxfam ya Kimataifa, Kongamano la Umoja wa Kimataifa juu ya Biashara na Maendeleo (UNCTAD) na Benki ya Dunia. Ili kupata orodha kamilifu ya machapisho, tafadhali tazama kiambatisho juu ya Makala za Kusoma (hapo chini).

5. *Hakuna mashauriano ya maana na Jamii.* Katika baadhi ya visa, jamii hazikushauriwa hata kidogo kabla ya ardhi yao kutolewa kwa mwekezaji. Katika visa vingine, mashauriano yalikuwa ni ya kiishara tu au hayakuhusisha uwakilishi mpana wa jamii, hasa wanawake. Hii hasi ni kutokana na ukosefu wa uwiano kiuhusiano kati ya maakida, viongozi wa kijadi, wakulima wadogo na jamii. Wafugaji, hasa, huelekea kutoonekana, hata kama wanahatarisha kupoteza haki yo ya ardhi muhimu ya malisho, kuni, maji na vifaa vingine vinavyotokana na misitu.
6. *Athari hasi kuu hasa kwa wanawake.* Katika Afrika chini ya Sahara, wanawake wana haki hafifu ya umiliki wa ardhi kuliko wanaume na hawahusishwi katika vikao vya kufanya maamuzi na mashauriano ya kijamii. Iwapo jamii itapokea fedha za fidia, mara nyingi wanawake hawafaidi kutokana nazo. Uhamishwaji na kupewa makao upya huongeza msongo kwa haki dhaifu za wanawake kwa ardhi. Hili pia huweza kudhoofisha uwezo wa wanawake kutimiza dhima yao ya kimsingi kama wazalishaji wa chakula cha matumizi ya nyumbani. Utafiti wa Taasisi ya Kimataifa juu ya Sera ya Chakula (IFRPI) unaonyesha kwamba wanawake aghalabu hutegemea pakubwa kwa raslimali za umma, kama vile misitu na vyanzo vya maji, na hivi ndivyo hulengwa na wawekezaji. Athari kwa wanawake pia ni muhimu katika muktadha wa madaliko ya tabia nchi, kwa sababu athari ya mafuriko na ukame huathiri uwezo wa wanawake kuzalisha chakula kwa ajili ya familia zao na mahitaji mengine ya kinyumbani.
7. *Ni nadra wawekezaji walitimiza miadi yao* kwa mujibu wa kutoa faida kwa nchi kupitia kubuni nafasi za kazi, uhamishaji wa teknolojia na ustawishaji wa miundo mbinu. Kufikia sasa, kuna ubunaji mdogo sana wa nafasi za kazi kutokana na miradi hii ya uwekezaji. Mara nyingi, nafasi za wafanyi kazi huchukuliwa na mashine, wakulima hawawezi kupata kazi na wawekezaji huwaajiri watu wanaolipwa ujira mdogo wanaotoka kwingine. Nchini Ghana, kwa mfano, kuna kisa ambapo jamii iliahidiwa kazi wakati wa mchakato wa mashauriano, lakini ahadi hii ya kazi haikutimizwa.
8. *Ukosefu wa mwoano kati ya mikakati* ya kitaifa kuhusu maendeleo na upunguzaji wa umaskini. Kwa jumla, mipango ya miradi haikuandaliwa vizuri na haikuhusiana kwa vyovyote na mikakati ya maendeleo kitaifa. Nchini Tanzania, kwa mfano, kuna mwekezaji aliyeharakisha mradi wa fueli za bio ilhali serikali haikuwa na sera kuhusu fueli za bio. Kuna ongezeko la habari kuhusu uchangamano wa uwekezaji wa aina hiyo na kutokuwepo kwa desturi nzuri ambazo zinaweza kusaidia kufikia hali ya ushindi kwa wawekezaji, serikali na jamii. Ukweli ni kamba uwekezaji hauleti mchango chanya kwa maendeleo kisadfa, bali unafaidi kutokana na maandalizi kimaksudi; kupitia kwa sera nzuri, desturi nzuri na mazingira mazuri kisheria.
9. *Nchi zina wajibu wa kuheshimu, kulinda na kutimiza haki za kibinadamu.* Hili hutokea sio tu kwa watu wanaoishi ndani ya mipaka yao bali hata kwa wale wanoishi nje. Zaidi ya robo ya watu wote duniani hawana ardhi, wakiwemo watu milioni 200 ambao huishi maeneo ya mashambani; licha ya ukweli kwamba ardhi ndio tegemeo kuu la maisha ya watu mashambani. Athari za haki za kibinadamu kutokana na unyakuzi wa ardhi ni pamoja na kuleta umaskini, maradhi na hata upotezaji wa maisha.

Baadhi ya washiriki pia walielezea tajriba zao chanya:

1. Nchini Angola, kwa mfano, serikali inafanya kazi kwa karibu na jamii na sekta ya kibinafsi ili kuifanya ardhi iwe na faida zaidi, hasa katika uzalishaji wa chakula, na hili lina athari chanya juu ya umaskini.
2. Nchini Zambia, kuna miradi ambapo wawekezaji wanatumia wafanya kazi wa humo nchini, lakini mazao yote huuzwa nje ya nchi.
3. Nchini Togo, mbunge mmoja, ambaye jimbo lake liko katika eneo lenye migodi, alilalamika kuhusu wawekezaji wa machimbo na athari hasi kwa jamii. Katika kujibu, serikali iliamua kusatwisha sheria za maadili mema kwa sekta ya machimbo, sheria ambayo ingesaidia kuboresha kiwango cha uwekezaji katika nchi.

4. Nchini Liberia, bunge huidhinisha mikataba yote inayohusu ukodishaji wa ardhi kati ya nchi na wawekezaji wa nje, na mapatano haya huchapishwa kwenye tovuti. Hii ndio desturi bora zaidi iliyowahi kuripotiwa barani, ikihakikisha kwamba kuna uangalizi wa bunge na uangavu kwa wananchi.



From left to right, Hon. Sisa James Njikelana from South Africa, Mouhamet Lamine Ndiaye from Oxfam Great Britain in West Africa, Angela Mulenga from the Foodfirst Information and Action Network (FIAN) in Zambia, and Hon. Bernadeta Mushashu from Tanzania discussing the impacts of foreign investment on farmland and water. *Photo courtesy of Ruth Hall, PLAAS*

## *Athari Kisheria kwa Uwekezaji wa Kigeni*

Kuna vyanzo vitatu vya sheria ambavyo ni muhimu kwa uwekezaji wa kigeni katika ardhi ya kilimo na maji. Kwanza ni Sheria za kinyumbani na kanuni za nchi mwenyeji. Hiki ndicho chanzo cha kimsingi cha sheria ambazo zinafaa kutumiwa ili kuendesha uwekezaji. Lakini, katika nchi nyingi, sheria hizi ni dhaifu mno, hasa kuhusiana na haki za ardhi za jamii za kijadi.

Chanzo cha pili cha sheria ni mkataba wa uwekezaji kati ya mwekezaji wa kigeni na nchi mwenyeji, ambacho pia huitwa Mkataba wa Serikali mwenyeji. Hizi sheria huweka bei, kiasi na muda wa ununuzi au ukodishaji, pamoja na masuala mengine yanayojumuisha motisha kwa mwekezaji, haki ya kuuza mazao nje mahitaji ya miundo mbinu mingine kutoka kwa serikali au mwekezaji, mahitaji ya kimazingira, na maendelo kiuchumi na kimaendeleo pamoja na muungano kati ya jamii ya jadi na uchumi. Mikataba ya uwekezaji aghalabu huibuka kuwa kanuni kisheria kwa uwekezaji. Zinaweza kupambanua ni sheria zipi zitafuatwa kukitokea mabishano, na hata kuzuia sheria za kijadi ambazo zingetumika wakati wa kuwekeza, kupitia kwa ujumuishaji wa "masharti ya uthabitishaji".

Chanzo cha tatu cha sheria ni Mkataba wa Uwekezaji wa Kimataifa. Hii ni mikataba ya pande mbili ambayo inawapa wawekezaji wa kigeni ulinzi wa kipekee chini ya sheria ya kimataifa. Zinatoa haki na "tiba" anuai kwa mwekezaji mbali na zile zilizopo katika sheria za kijadi au katika mkataba. Mingi ya mikataba hii huwa na mchakato maalum wa usuluhishaji wa mabishano unaoitwa upatanishi kati ya mwekezaji na serikali.

Haki zilizobainishwa katika mapatano na mkataba zinaongezwa juu ya sheria za kijadi, ambayo ni lazima ioane na masharti. Vyanzo hivi viwili vya sheria huanza kutoka kwa mwelekeo wa kibiashara kwa nia ya kulinda maslahi ya mwekezaji. Vinatoa haki thabiti za kimkataba na mbinu za upatanishi kwa wawekezaji wa kigeni dhidi ya msululu wa vitendo vya serikali. Hata hivyo, mara nyingi zinafeli kushughulikia wazi wazi maslahi kiuchumi na kijamii ya watumiaji wa kijadi au mielekeo ya kimazingira inayohusiana na uwekezaji.

a. Wanapata haki gani wawekezaji wa kigeni wanapowekeza?
   Kandarasi na Mikataba ya uwekezaji inaweza kuwapatia wawekezaji haki za ziada za kutumia maji, umiliki wa ardhi na haki ya kuuza nje ya nchi mazao yote. Mwekezaji ambaye anajumuisha sharti la kudumisha uthabiti katika mkataba huenda pia akaweza kukwepa kutekeleza sheria za nchi mwenyeji ambazo huenda zikabuniwa baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa mkataba. Isitoshe, kwa kukubali uwekezaji wa kigeni, kwa ujumla, nchi wenyeji hukubali kwamba zitatoa njia za kuwezesha utumikaji wa mikataba, kwa mfano, kuchota maji kwa ajili ya shughuli za kilimo. Kukubali huku hutuoa hakikisho la usalama, hata kama hakikisho hilo litakinzana na mahitaji yaliyopo au yajayo ya maji ya kunywa, ya kunyinyizia mashamba madogomadogo, viwanda vidogovidogo au matumizi ya kinyumbani kwa wenyeji.

b. Nini hutokea kwa haki za watumiaji wa awali?
   Iwapo sheria ya nchi ni wazi na imetungwa kwa kuihusisha na haki za wananchi ambao ni watumiaji wa ardhi, watu hawa watukuwa na haki ya kushirikishwa katika mchakato wa kuandaa mkataba. Tatizo ni kwamba katika nchi nyingi ambapo mikataba huandaliwa, haki za ardhi na maji ni tata, zimejikita katika tamaduni za kijadi au hazipo kabisa. Haki-miliki ni ya serikali, maakida wa kijadi au miundo mingine ya kijamii. Watumiaji halisi huwa hawana haki wazi wazi. Katika hali hiyo, mwekezaji huwa na haki zake za kimkataba anazozitumia kama ndizo haki thabiti na zinazostahili kutekelezwa.

c. Ni nini hutokea wakati ambapo sheria za kijadi zinabadilika?
   Ni nini kitatokea iwapo serikali itaanzisha sheria mpya za mazingira ili kuilinda dhidi ya madhara ya madawa ya kuua wadudu waharibifu wa mimea na mbolea, iwapo serikali itaharamisha kemikali fulani, au inaongeza kiwango cha chini kabisa cha ujira wa kulipwa? Mabadiliko katika sheria yanaweza kusababisha madai ya kukiukwa kwa mkataba au vipengele vinavyoilinda mikataba ya wawekezaji wa kigeni, na kutibua mabishano ambapo mwekezaji atadai fidia. Visa kadhaa vya upatanishi kati ya mwekezaji na nchi vinavyojulikana vinahusu mabadliko katika sheria za mazingira, sheria za kugawa katika zoni/kanda, viwango vya mirabaha na hatua nyingine ambazo zina athari kwa utekelezaji wa uwekezaji. Iwapo mkataba una kipengele cha "uthabiti" ambacho kinazuia uwezo wa serikali kutunga sheria mpya zinazoweza kuathiri uwekezaji, mahakama zitatilia maanani jambo hili katika kubainisha iwapo mkataba umekiukwa.



From left to right, Dr. Hubert Ouedraogo from the African Union - African Development Bank - UN Economic Commission for Africa partnership, Hon. Yawovi Henri Gbone from Togo and Carin Smaller from the International Institute for Sustainable Development, discussing the legal implications of foreign investment in farmland and water. *Photo courtesy of Ruth Hall, PLAAS.*

## *Hatua za Umoja wa Afrika na za kiulimwengu kuhusu kilimo, maendeleo ya mashambani, ardhi na maji*

a. Miongozo ya Sera kuhusu Ardhi ya Umoja wa Afrika

Usimamiaji mzuri wa ardhi ni kipengele muhimu kwa maendeleo ya Afrika. Miongozo ya Sera za Ardhi ya UA ni ishara ya kujitolea kwa utungaji wa sera ya ardhi, utekelezaji na ufuatiliaji wake. Miongozo hiyo inakuza maelewano na kusisitiza haja ya ushiriki wa watu wote. Inatoa mifano ya desturi bora na kuhimiza matumizi ya amani endelevu ya raslimali asilia. Uandalizi wa mifumo ya kusimamia ardhi ni muhimu katika kufikia mazingira mazuri kwa uzalishaji ulioimarika wa kilimo. Ulinzi na usimamiaji wa raslimali asilia, hasa maji, na vilevile maeneo ya malisho ya mifugo, ni muhimu sana.

Wabunge kadhaa walizungumzia mipango ya nchi zao katika kushughulikia shinikizo kwa ardhi. Nchini Angola, kwa mfano, kuna haja ya (1) kushughulikia hati-miliki za ardhi ya jamii na kutafuta iwapo wanajamii wanaitumia ardhi hiyo au la (2) kujadili utoaji wa bei kwa ardhi na mahitaji ya uzalishaji ili kufikia uwezo halisi; (3) kubuni mfuko kwa ajili ya vyama vya ushirika vya kijamii; na (4) kumteua Kamishna wa Haki za watu ambaye anaweza kutekeleza programu ya elimu kuhusu haki za kijamii kwa ardhi, haki za kiuchumi, kiraia na kisiasa.

b. Kanuni kwa ajili ya Uwekezaji Unaowajibika katika kilimo, na benki ya Dunia, FAO, IFAD na UNCTAD
Kanuni hizi zinajumuisha kuzingatia haki za ardhi, usalama wa chakula, haja ya uangavu na uongozi bora, kushauriana na kuwashirikisha wadua husika, uwekezaji wa kuwajibika, uendelevu kijamii na kimazingira . Kanuni hizo zinashindana kwa namna fulani na Miongozo ya Kujitolea ya FAO (hapo chini) lakini zimeshambuliwa kwa kutokuwa na mchakato wa kushauriana na njia ya ufuatiliaji ili kubainisha iwapo serikali na wawekezaji wanazingatia kanuni zilizowekwa. Zaidi ya yote, hatua hii, kwa kiasi kikubwa, inalenga tendo la mwekezaji kuliko serikali.

c. Miongozo ya Kujitolea ya FAO kuhusu Umiliki wa Ardhi
Huu ndio muundo mpana zaidi ambao umewahi kubuniwa. Sifa yake kuu ni kurejelea haki zilizopo za kibiadamu na mikataba, ikiyakumbusha mataifa wajibu wao. Masharti yake yanahusiana na mfumo wa usimamiaji wa umiliki ardhi unaowajibika, ikiwa ni pamoja na kutambua na kuheshimu watumiaji waliopo tayari na haja ya kuzingatia viwango vya kimataifa. Makubaliano yanatakiwa kutokana na idhini huru, inayotolewa awali baada ya kuelewa kinachohitajika. Nguzu za miongozo hii zinatokana na mchakato mpana wa pembe nyingi unaongozwa na Umoja wa Mataifa. Jamii ya kiraia imeshiriki katika mijadala hii, pamoja na serikali na sekta ya kibinafsi. Waraka huu unajaliza Miongozo ya Sera ya Ardhi ya UA. Dosari zao ni kwamba miongozo hii ni ya hiari, hivi kwamba si wazi zinaweza kuwa na athari gani. Waraka huu pia una udhaifu kuhusiana na haki za wanawake na masuala ya maji.

---

## *Uwekezaji wa Kilimo Kiumma na Kibinafsi: kutekelea Azimio la Maputo*

**a. Kuyafikia Madhumuni ya Azimio la Maputo**
Madhumuni ya Azimio la Maputo ni shabaha ya ukuaji katika sekta ya kilimo kwa 6% na 10% ya bajeti kutengewa sekta ya kilimo . Usalama wa chakula ni kitovu cha mipango ya uwekezaji ya CAADP, lakini kuna msisitizo kidogo katika usimamiaji endelevu wa ardhi na maji, sayansi na teknolojia, na ni kana kwamba hakuna kurejelea “unyakuzi wa ardhi”. Kwa sasa kuna jaribio la kutenga 6% ya bajeti kwa usimamiaji wa raslimali za ardhi na maji. Nchi saba ama zimetimiza au kuzidi shabaha, zikiwa ni Guinea, Senegal, Burkina Faso, Malawi, Mali, Niger na Ethiopia. Kwa wastani, nchi za Kiafrika zilitenga 6.5% ya bajeti zao za kitaifa kwa kilimo, ilhali wastani ya Afrika chini ya Sahara ilikaribia shabaha ya 9% nayo ECOWAS ilifikia wastani ambayo ni juu kuliko mgawo wa 10%.

**b. Kufaa kwa Ufadhili, Jinsia na Uwekezaji katika Kilimo**
Msaada wa Maendeleo kwa Nchi za Nje (ODA) haujafikia madhumuni yake. Msaada huu kwa nchi za Afrika ulifikia kiwango cha juu kabisa cha $ bilioni 7.6 mnamo 2009 na ilikadiriwa kuwa na ongezeko la 4% katika 2010, ingawa shabaha bado hazijafikiwa. Programu nyingi za misaada ya kilimo zinafeli kujumuisha tathmini ya kimsingi kijinsia, na jinsi maingilio kati yaliyopendekezwa yatakavyowaathiri wanaume na wanawake kwa njia tofauti. Kushughulikia pengo kijinsia katika kilimo na maendeleo ya mashambani huweza kuwa na athari nyingi kwa afya, raha na ustawi, ukuzaji wa mtaji watu na ustawi kiuchumi. Katika sekta ya kilimo, hii ina maana kwamba wanawake watakuwa na haki sawa na wanaume ya kununua, kuuza, kurithi ardhi, kufungua akaunti za kuhifadhi na kukopa pesa, kusaini mkataba na kuuza mazao yao. Kwa jumla, Afrika inahitaji kupunguza utegemezi wake kwa Msaada wa Maendeleo kwa Nchi za Nje (ODA), hasa kwa kuzingatia janga kuu la kifedha lililokuwepo. Tunahitaji kupiga hatua kutoka kwa kufaa kwa ufadhili na kuanza kufikiria kufaa kwa maendeleo.

c. Mitindo mbadala kibiashara ya kuwekeza katika kilimo

Kilimo kinahitaji kujumuisha mitindo ya kibiashara ili kushughulikia changamoto fiche za uzalishaji wa ardhi. Kwa kuzungumzia miradi ya uwekezaji moja kwa moja na watu wa nchi mnamowekezwa, kuna uwezekano wa kuimarisha haki za ardhi na maji, kupunguza migogoro katika jamii za jadi, kukuza ufumbuzi wa ushindi kwa pande zote, na kuhakikisha tahadhari kijamii na kimazingira. Kuna mitindo ya kibiashara kadhaa inayojumuisha miradi ya pamoja, ukulima kwa mkataba au mipango ya kilimo kinachofanywa na wakulima wadogo lakini wakauzia kampuni kubwa, mikataba ya usimamiaji, miungano ya kwenda juu na chini, na biashara zinazomilikiwa na wakulima.

*Miradi ya Pamoja* inahusu umiliki wa pamoja, kugawana hasara na faida, kufanya uamuzi na migawo ya faida kulingana na uwiano wa mgawo wa uwekezaji, huku wenye hisa chache wakiwakilishwa katika kufanya uamuzi. Jamii zinaweza kuchangia kwa ardhi na maji kama raslimali yao, lakini iwapo hii haitathminiwa, basi udau wao hautalingana na thamani ya mchango wao. Wanunuaji aghalabu huweka bei na hali hii huweza kuzua uhusiano usio sawa wa mamlaka.

Mitindo ya kibiashara ambayo ni jumuishi si mpango wa maendeleo. Inaweza kuwa vigumu wakati ambapo unajaribu kupata fidia kutokana na kuipanua biashara na huenda ikaongeza gharama za kuendesha biashara kwa sababu ya haja ya kufanya kazi na washirika zaidi. Lakini mitindo hii inaweza kuleta faida kupitia kwa shughuli za kimsingi za kibiashara na wala si kupitia uhisani, na hatimaye inaweza kuhakikisha kuwepo kwa msambao sawia kifedha, kijamii na kimtaji asilia kati ya wawekezaji na watu wa nchi mnamowekezwa, kupitia kwa msululu wa soko.




From left to right, Ousmane Djibo from the Comprehensive Africa Agriculture Development Programme (CAADP) and Rosalie Lo from the New Economic Partnership for African Development (NEPAD), discussing public and private investment in Africa, aid effectiveness, and the implementation of the Maputo Declaration. *Photo courtesy of Ruth Hall, PLAAS.*

## *Nafasi ya Wabunge*

Wakati wote wa semina, washiriki walilenga hasa nafasi ya wabunge katika kuitikia kukua kwa uwekezaji wa kigeni katika ardhi ya kilimo na maji. Majukumu kadhaa ya kimsingi yalibainishwa, lakini wabunge walisisitiza kwamba hawangeweza kuifanya kazi yote peke yao., bali walihitaji ushirikiano na wakala wa Afrika nzima, AU-ECA-AfDB nad NEPAD, pamoja na mashirika ya Kiafrika na kimataifa ya jamii za kiraia, kama vile Jukwaa la Afrika, IISD, Oxfam-Afrika Magharibi, FIAN-Afrika, IDASA, PLAAS, IIED, ILC na wengine. Kulitolewa mwito wa kuzindua kampeni za kitaifa, kikanda na kibara ambazo zitahusu sio mageuzi kisheria tu bali pia kampeni za kisiasa ambazo zinaratibiwa katika kiwango cha bara zima ili kuruhusu uanzishwaji wa maadili mapya ya uwekezaji.

Dhima kuu ya wabunge itajumuisha:

- Nafasi ya uangalizi ili kuhakikisha ujumuishaji kijamii na uangavu wa miradi ya uwekezaji: kuzishinikiza serikali kutoa fursa ya kufikia habari, kuitikia na kupendekeza lugha mbadala katika mikataba; na kuingiza masharti ya kuwalinda watu wetu.
- Kufanya kazi kama watunga sheria, wafuatiliaji wa sera za serikali na walinzi wa maslahi ya umma; kutunga sheria za kuifanya lazima kuwa na idhini ya hiari, ya kabla na inayotakana na ufahamu wa jamii ndiposa mikataba ya uwekezaji itiwe saini; kuanzisha kamati za kutathmini desturi na uendeshaji wa biashara; na kufuatilia uzingatiwaji wa miadi ya biashara na athari ya miradi ya uwekezaji.
- Kuwa wafanya maamuzi kisiasa na kutozingatia mirengo ya kivyama: kuweka kipaumbele katika kujenga uwezo wa raia ili wawe wapatanishi, huku wabunge wakiwa wenzi wao; kutozingatia vyama vya kisiasa kwa manufaa ya wote.
- Kuzigeuza sera kuwa vitendo halisi katika viwango vya kitaifa na kijadi: kuandaa miongozo juu ya uongozi mwema wa ardhi kwa kuunga mkono Hatua ya UA kuhusu Sera ya Mwongozo juu ya Ardhi.
- Kufuatilia utekelezaji wa Miongozo ya Sera ya UA kuhusu Ardhi na Azimio la Maputo lenye shabaha ya 10%; kutumia udhibiti wa wabunge juu ya migao ya bajeti ili kushawishi sharti la mgawo mkubwa kutengewa sekta ya kilimo.
- Kutetea, kuzuia na kufichua desturi za ufisadi.



From left to right, Isilda Nhantumbo from the International Institute for Environment and Development, Hon. Adeo Crenstozao Neto from Angola, and Hon. Dr. Augustin Iyamuremye from Rwanda. *Photo courtesy of Ruth Hall, PLAAS.*

## *Mapendekezo na hatua fuatilizi*

a. *Kuboresha Uangavu.* Wabunge wana nafasi muhimu ya kuzihimiza serikali kuitoa mikataba wazi kwa umma. Kuna mwelekeo unaozidi kuwa maarufu duniani wa kuwa waangavu kuhusu mikataba ya umma. Mnamo 2011, Shirika la Kimataifa la Wanasheria na Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Watu, alitaka kuwepo na uangavu katika mikataba. Kanuni za Benki ya Dunia kwa ajili ya Uwajibikaji katika Uwekezaji katika Kilimo zinataka kuwepo kwa uangavu wa kufikia ardhi na uwekezaji. Mwandishi maalum wa Umoja wa Mataifa juu ya haki kwa chakula, ametaka kuwe na uangavu kamili katika mikataba ya ardhi na ununuzi. Liberia inaongoza njia na iliamua katika sheria yake ya uanganvu kuhusu uwekezaji mnamo 2009, kwamba watachapisha mapatano na mikataba yote katika sekta za machimbo, kilimo,misitu na mafuta. Nchi nyingine zinafaa kuiga hatua hii.
b. *Mageuzi ya Ardhi.* Ukosefu wa usalama katika haki za ardhi katika Afrika umeruhusu hali hii kutokea. Tiba iko katika utambuzi kisheria kwamba haki za kijadi za ardhi ni sawa sawa na haki halisi za mali. Bila mabadiliko haya ya kisheria, jamii zitabaki kuwa za maskwota katika ardhi yao. Mageuzi ya ardhi yanaweza kufanywa na kupitia kwa uwezeshaji wa usimamiaji wa ardhi mashinani. Ni lazima serikali zigatue mamlaka yao juu ya ardhi kwa jamii ambazo zinamiliki ardhi. Taasisi za mashinani zinahitaji kuwa na demokrasia na kustawishwa ili kuunga mkono mchakato huu (kama inavyotokea katika Afrika Kusini, Msumbiji na Angola). Ni lazima mamlaka za kijadi zifanyiwe mageuzi ili kuhakikisha uwakilishaji mwafaka wa jamii. Sheria za taifa juu ya haki kwa ardhi, maji na raslimali nyingine ni lazima zielezwe wazi wazi kwa watumiaji wazo. Isitoshe, serikali na mabunge zinatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kustawisha mpango wa matumizi ya ardhi na kuandaa orodha ya ardhi iliyopo.

c. *Mashauriano halisi na jamii,* yanayojumuisha idhini yao huru, ya awali na inayotokana na ufahamu wao ndiposa mikataba ya uwekezaji itiwe saini.

d. *Kujenga Ufahamu na Uwezo juu ya Uwekezaji wa Kigeni.* Kuna haja ya kuhisisha umma juu ya kampeni ya kujenga uwezo ili watu wajue haki zao, waweze kufikia miradi yao ya uwekezaji, na wale na stadi za kufanya majadiliano kwa kutegemea ujuzi na utaalamu. Bunge la Afrika na washirika wake linafaa kuzindua warsha za kikanda kwa wabunge na jamii za kiraia; kuziwezesha jamii pale ambapo uwekezaji wa kima kikubwa unafanyika; na kustawisha uwezo wa serikali na wamiliki wa kijadi wa ardhi kuelewa thamani ya raslimali zao na kuweza kujadiliana na wawekezaji wao.

e. *Kuanzisha na kuimarisha Vituo vya Utaalamu wa Juu kuhusu Ardhi, Kilimo na Raslimali Asilia.* Kuna utafiti unaotegemea ushahidi, unaojumuisha uwekezaji, ni wapi pana miradi, fedha na athari (tazama kiambatisho Reading Materials). Pia kuna miundo ya kimataifa na kikanda ambayo inaweza kuhudumu kama marejeleo ya miongozo kuhusu uwekezaji wa kigeni ( Miongozo ya Sera kuhusu Ardhi ya UA, Miongozo ya Hiari ya FAO, Kanuni za Benki ya Dunia, nk.). IISD ina mtindo wa mkataba wa uwekezaji ambao ni kifaa muhimu cha kutumiwa. Michakato miwili ya kimataifa imeandaa kanuni zinazotumiwa katika mikataba ya uwekezaji. Hii inafaa kuwa msingi wa ustawishaji zaidi wa vituo vya utaalamu katika Afrika.

*f. Kukataza kwa Muda Unyakuzi wa Ardhi.* Miradi mikubwa ya ardhi inafaa kuchukuliwa kuwa hatua ya mwisho na kipaumbele kitolewe kwa kilimo cha wakulima wadogo wadogo na mitindo mingine mbadala ya uwekezaji wa ushirikiano kati ya jamii na mwekezaji. Washiriki kadhaa walihisi kwamba ni muhimu kukataza kwa muda unyakuzi wa ardhi wa kima kikubwa. Walikuwa wanaunga mkono kampeni ya Afrika nzima inayotaka usitishwaji wa muda hadi wakati ambao muundo mwafaka utakuwa umepatikana na ambao ungeiwezesha Afrika kufaidi kutokana na wimbi la sasa la uwekezaji. Wengine walikuwa na tahadhari, wakidai kwamba ilikuwa afadhali kutafuta njia za kufanya uwekezaji wa kufana katika Afrika, kuliko kuomba usitishwaji wa muda.

---

## *Rasimu ya Azimio*

Sisi, wanachama wa Kamati juu ya Kilimo, Raslimali Asilia, Uchumi wa Mashinani na Mazingira wa Bunge la Afrika, Bunge la Taifa la Jamhuri ya Angola, Bunge la Taifa la Jamhuri ya Benin, Bunge la Taifa la Jamhuri ya Burkina-Faso, Bunge la Jamhuri ya Ghana, Bunge la Taifa la Jamhuri ya Kenya, Bunge la Taifa la Jamhuri ya Sudan, wawakilishi wa Jukwaa la Afrika, IDASA, Hatua ya Sera ya Ardhi ya AUC- ECA- AfDB (LPI), Wakala wa Upangaji na Uratibu wa NEPAD, "Centre de coopération internationale en recherche agronomique pour le développement", Habari kuhusu Chakula Kwanza na Mtandao wa Vitendo, Taasisi ya Kimataifa kwa ajili ya Mazingira na Maendeleo, OXFAM na Taasisi ya Taaluma za Umaskini, Ardhi na Kilimo.

**Baada ya** kuhudhuria Warsha ya Bunge la Afrika yenye dhamira *Kufanya Uwekezaji uwe na Manufaa katika Afrika: Maitikio ya Mbunge kwa "Unyakuzi wa Ardhi";*

**Tukitambua haja ya kuwekeza katika** maendeleo ya Afrika hasa katika kilimo na katika maeneo ya mashambani ambapo watu wengi huishi;

**Tukielewa kwa masikitiko sana** unyakuzi wa vipande vikubwa vya ardhi hivi majuzi ambao pia unaitwa "unyakuzi wa ardhi" na athari yake kijadi na kwa Uwekezaji wa moja kwa moja wa Kigeni katika ardhi, maji na raslimali asili zinazohusiana;

**Tukigutushwa vilivyo** na athari hasi kwa haki za watu hasa wanawake, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa kuifikia ardhi kisawia na kuvuruga uwezo wa kuyafikia maji;

**Tukisumbuliwa sana** na ukame ambao haujawahi kuonekana katika Upembe wa Afrika na athari zake kwa watu wetu;

**Tukitambua** umuhimu wa kulinda na kukuza uwiano na haki miongoni mwa watu wetu;

**Tukikubali** Muundo wa Umoja wa Afrika na Miongozo kuhusu Sera ya Ardhi Afrika, Azimio la Maputo kuhusiana na ACHPR juu ya Haki za Wanawake katika Afrika na Azimio la Dhati kuhusu Usawa KiJinsia katika Afrika;

**Tukisisitiza** Azimio la Maputo la 2003 kuhusu Kilimo na Usalama wa Chakula katika Afrika, hasa kujitolea kutenga angalau 10% ya bajeti ya raslimali za kitaifa kwa kilimo na utekelezaji wa sera ya maendeleo ya mashinani;

Tunaazimia:

1. Kuendesha hoja ya azimio la kuziomba Nchi Wanachama kuitikia hali hii kwa dharura na kwa hivyo kutaka Tume ya Umoja wa Afrika na Wakala wa Kuratibu na Kupanga wa NEPAD kuongoza juhudi hii.
2. Kuomba usitishwaji kwa muda unyakuzi mpya wa ardhi kubwa kubwa tukisubiri utekelezaji wa sera za ardhi na miongozo juu ya desturi nzuri za usimamiaji wa ardhi.
3. Kuomba uandalizi wa *Kongamano la Mawaziri wa Afrika kuhusu Uwekezaji wa Ardhi* katika kiwango cha Kongamano la Mawaziri wa Mazingira (AMCE) na Baraza la Mawaziri kuhusu Maji (AMCOW).
4. Kuomba utungaji wa sera madhubuti za ardhi ambazo zinatambua na kulinda haki za raia kama sharti la mazungumzo yoyote kuhusu uwekezaji.
5. Kuomba uandalizi na utekelezaji wa miongozo juu ya usimamiaji bora wa ardhi ili kuimarisha kanuni za maadili kwa Uwekezaji wa moja kwa moja katika Afrika.
6. Kuomba kanuni za Uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika ardhi na raslimali asilia zinazohusiana nayo, kujenga juu ya hatua zilizopo za UA, FAO na Benki ya Dunia ili kulinda faida za uwekezaji kwa watu wa Afrika na kukuza hali endelevu za maisha. Hii ni pamoja na:
    a. Masharti ya lazima kisheria na yanayoweza kulazimishwa kwa wawekezaji kuchangia uchumi na afya kijamii katika nchi wanamowekeza;
    b. Kupunguza viwango vya umaskini, kuboresha usalama wa vyakula, na kuyalinda mazingira;
    c. Kuongeza idadi na hali ya watu wanaoajiriwa na kujenga uwezo na kuboresha miundo mbinu na zuhawilisha teknolojia.
    d. Kuhakikisha mashauriano ya kufaa na jamii za nchi mnamowekezwa na watu anuai wanaoathiriwa na miradi ya uwekezaji na kuhakikisha kwamba uwekezaji wowote unapitishwa na jamii inayohusika baada ya idhini ya hiari, ya kabla na inayotokana na ufahamu wao;
    e. Kuimarisha mfumo wa uthibitisho na uandikishaji wa ardhi unaozingatia mifumo anuai ya kilimo; yaani haki za wafugaji, haki za wanawake na haki za kijamii, kabla ya uwekezaji katika ardhi kufanywa.
7. Kuhakikisha kwamba serikali zinawajibika kwa uangavu zaidi wa kuifichua hadharani bila kuchelewa, mikataba ya uwekezaji.
8. Kuunga mkono mchakato wa warsha za kikanda kwa wabunge, wanasiasa, jamii za kiraia, mashirika ya wakulima na utafiti, ili kukuza ufahamu kuhusu unyakuzi wa ardhi kubwakubwa.

9. Kujitolea kuunga mkono hatua za Kiafrika za kujenga ufahamu miongoni mwa mabunge ya kitaifa, wananchi na jamii zinazoathiriwa.Garantir mecanismos mais fortes para monitorização e aplicação das leis nacionais, acordos regionais e tratados e convenções internacionais.
10. Kuhakikisha kuna mbinu zenye nguvu za kufuatilia na kutekeleza sheria za kijadi, mikataba ya kikanda na Mikataba na mapatano ya kimataifa.
11. Kuunga mkono vituo vya utaalamu vikiwemo taasisi za utafiti ili kurekodi uwekezaji unoajikita katika ardhi unaokuja na kutumia pamoja habari kwa njia rahisi ya kupatikana kwao na watunga sera, wabunge, jamii za kiraia na jamii zilizoathiriwa.

Midrand 22 Julai 2011